

Uwezeshaji wa wanawake kiuchumi barani Afrika

Ufumbuzi unaowezekana kutoka kwa tathmini za athari

Kupunguza pengo la kijinsia katika soko la ajira ni muhimu katika kuhakikisha uwezeshaji wa wanawake kiuchumi. Licha ya kurekodi moja ya kiwango cha juu zaidi cha ushiriki kazini, wanawake wa nchi za Afrika zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara bado wanakabiliwa na vikwazo vingi vya kitaasisi, kiuchumi na kitamaduni ambavyo vinasababisha upatikanaji mdogo wa malipo, ajira rasmi na mapato ya chini, kudhoofisha uwezo wao wa kuwa na utulivu na uhuru.

Kwa kutumia mifano mingi kutoka nchi za Afrika zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara, hati hii inakusanya ushahidi na masomo tuliyopata kuhusu jinsi ya kushinda vikwazo hivi na kupunguza ipasavyo pengo la kijinsia katika soko la ajira. Maoni yanalenga tu ushahidi kutoka kwa tathmini za kisayansi kwa kutumia mbinu za majaribio au zinazoonekana kuwa za majaribio, na ambayo huturuhusu kubainisha athari ya afua zilizojaribiwa.

Vikwazo vya kijamii na kitamaduni vinazuia upatikanaji wa kazi na tija kwa wanawake

Fursa na matokeo ya kiuchumi ya wanawake yanabanwa sana na anuwai za kanuni za kijamii na kitamaduni, kama vile mzigo wa kazi za nyumbani, mwingiliano wa kijamii uliozuiliwa, na dhana potofu za kijinsia. Kwa hakika, muda ambao wanawake hutumia katika utunzaji wa kaya unashindana na muda wanaoweza kujitolea kwa mafunzo, uanagenzi na shughuli za kuzalisha kipato (IGA), na hivyo kuzorotesha tija yao. Ushiriki huu pia unazuiwa na kanuni za kijamii zinazozua mwingiliano nje ya kaya zao. Hatimaye, majukumu madhubuti ya kijinsia ya kitamaduni na fikra potofu mara nyingi huchukuliwa kwa uzito na wanawake na kuwa na athari kubwa katika kujiamini na ushindani wao, na hatimaye katika chaguzi zao za kitaaluma na kazi.

Ufumbuzi wenyewe kutegemeka umetambuliwa kupitia tathmini ya kina ya athari kote Ulimwenguni

Ufumbuzi wa 1: Toa huduma za utunzaji watoto na ratiba zinazonyumbulika

Wanapokabiliwa na changamoto ya mzigo wa kazi za nyumbani, kutoa huduma za utunzaji watoto kunaweza kuongeza tija ya wanawake, kupata mafunzo na kufanya kazi nje ya nyumbani. Tathmini za athari zimeonesha kuwa kutoa ufikiaji au kutoa ruzuku kwa huduma za utunzaji watoto kuliongeza viwango vya ajira vya walezi kwa takriban 26% nchini Msumbiji na 17% nchini Kenya. Kusini mwa Togo, kuandikisha watoto wa miaka 3 hadi 5 katika shule za chekechea kulifanya wanawake kuwa na uwezekano wa 37% wa kufanya kazi nje ya nyumbani. Nchini Burkina Faso, vituo vya kutunza watoto vya kijamii viliruhusu wanawake wanaowalea watoto wa chini ya miaka 2 kutumia muda wa 20% zaidi katika ajira ya kulipwa na kuleta ongezeko la 50% la mapato yao kutokana na kazi ya kulipwa.

Vile vile, programu ya shamba shuleni nchini Kenya, Tanzania na Uganda iliongeza uzalishaji wa mazao na mapato ya kila mtu kwa kaya zinazoongozwa na wanawake, kutokana na ratiba iliyoundwa na inayonyumbulika ambayo iliwezesha ushiriki wao kwa kuzingatia kazi za nyumbani.

Ufumbuzi wa 2: Tumia teknolojia mpya kukuza mafunzo na tija ya wanawake

Mafunzo ya nyumbani kwa kutumia kompyuta, Ujumbe mfupi au video hupunguza muda na gharama za usafiri za kupata habari, kuwezesha mafunzo bila uhitaji wa kushirikiana na mkufunzi wa kiume, na kuruhusu ushauri ubinafsishwe. Nchini Ethiopia na Uganda, vipindi vifupi vya video vilivyo husisha wakulima wakitekeleza mbinu mpya za kilimo viliwasilishwa kwa kaya kama sehemu ya programu ya mafunzo ya kilimo cha mahindi. Tathmini ya athari ilionyesha kuwa ushiriki uliongeza uwezo wa wanachama wa kike kupata habari kwa takriban 25% na kiwango cha kubakia na habari. Nchini Uganda, wanawake walikuwa na uwezekano mkubwa wa kufuata mazoea mapya yaliyopendekezwa. Nchini Ghana, ushauri wa uchunguzi wa kompyuta na uliobinafsishwa kila wiki kuruhusu mbinu za kilimo uliongeza maarifa ya wanaume na wanawake na kupitishwa kwa mbinu za kilimo lakini si faida. Kama sehemu ya utafiti mwingine nchini Niger, watu wazima wanaonufaika walipata mafunzo ya kuboresha mazao mbalimbali ya kilimo, pamoja na rununu ya kushiriki na wengine wanne wanaonufaika. Kilimo cha bamia, zao linalolimwa na wanawake hasa kiliongezeka.

Ufumbuzi wa 3: Kuajiri wakufunzi wa kike

Kuajiri wakufunzi wa kike kunaweza pia kusabisha mafunzo na kozi kupatikana kwa wanawake wakati mwiningiliano na wenza o wakiumenje yakaya ha kubaliwi. Serikali ya Msumbiji iliajiri washauri wanawake wa kujitolea ili kuunganisha wakufunzi wa kilimo katika mbinu za Usimamizi Endelevu wa Ardh (SLM) na kaya katika jamii zao. Walihimizwa kukuza na kusambaza mbinu walizojifunza kutoka kwa mawakala wa mafunzo katika mitando yao ya kijamii. Tathmini ya athari ilionyesha kuwa ujuzi wa wanawake wa SLM uliongezeka kwa karibu theluthi mbili kutoka kiwango chao cha awali na kupitishwa kwa SLM ya wanawake kuliongezeka kwa takriban 50%.

Ufumbuzi wa 4: Kutoa mafunzo kwa wenzi wa ndoa

Kualika wenzi wa ndoa kwenye mafunzo ya kilimo pia kumeonyeshwa kuwa muhimu katika kuboresha ushiriki wa wanawake katika uzalishaji, kuongeza tija ya kilimo ya kaya na wakala wa wanawake. Nchini Kodivaa, mafunzo ya siku 3 kuruhusu kilimo cha mbegu za mpira yalirolewa kwa wakulima na wenzi wao pamoja: Wakulima waliochukuliwa kama wenzi wa ndoa walionyesha usimamizi bora wa shamba, walitumia pembejeo ya kazi na isiyo ya kazi na walikuwa na uwezekano wa 19% kubaki na mpango wao wa kazi miaka miwili baada ya mafunzo. Walipanda miti maradufu na waliweza kudumisha viwango vya mavuno na tija kwa miti ya zamani, kinyume na mkulima mmoja mmoja ambao waliona mavuno yakishuka kwa 26%.

Ufumbuzi wa 5: Sahihisha dhana potofu kuhusu mapato na kanuni za kijamii zinazotambulika

Kusahihisha dhana potofu kuhusu mapato na kanuni za kijamii zinazotambulika kunawezakuwa kigezo chenyenguvi cha kurekebisha dhana potofu za kijinsia katika soko la ajira. Chaguo la tasnia huamuliwa na vipengele vingi kama vile dhana kuhusu malipo katika kila tasnia, pamoja na dhana kuhusu kanuni za kijamii. Katika nchi za Afrika zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara, wanawake wanaomilili biashara katika sekta zinazotawaliwa na wanawake wanapata faida ndogo, wana uwezo mdogo wa ukuzi na mara nyingi wako katika mazingira yasiyo rasmi ikilinganishwa na wanawake katika sekta zinazotawaliwa na wanaume kutoka jadi.

Tafiti mbili nchini Ethiopia na Uganda ziligundua kuwa wajasiriamali wanawake katika sekta zinazotawaliwa na wanawake huwa na tabia ya kudharau faida inayopatikana na wanawake katika sekta zinazotawaliwa na wanaume. Athari ya kusahihisha dhana hizi ilitathminiwa katika Jamhuri ya Kongo kama sehemu ya programu ya kukuza ujuzi. Kutoa taarifa halisi ya mapato na mishahara ya wastani ya kazi tofauti kuliongeza uwezekano kwamba mwanamke angechagua mafunzo katika sekta zinazotawaliwa na wanaume kama vile topografia na uendeshaji wa kreni, kwa 28%.

Zaidi ya hayo, uungwaji mkono kutoka kwawananafamilia wa kiume au marafiki ni sababu kuu ya wanawake kuingia na kuendelea katika nyanja zinazotawaliwa na wanaume. Wakati utafiti wa hivi majuzi wa AFD ulionyesha kuwa wanaume nchini Tunisia wanakadiria kwa usahihi hali ya kijamii inayowazunguka wanawake katika soko la ajira baada ya kusahihisha upendeleo wa kuhitajika, utafiti nchini Saudia ulionyesha kuwa waume wa wanawake wenye umri wa kufanya kazi hudharau kukubalika na jamii kwa mwanamke anayeingia katika soko la ajira. Walipofahamishwa kwamba wengi wa raia wenzao wa kiume walikuwa wanawapendelea, waume walikuwa na uwezekano mara 2.6 zaidi wa kuwaruhusu wake zao kufanya kazi nje ya nyumbani, na wake zao walikuwa na uwezekano mkubwa zaidi wa kutuma maombi ya kazi.

Ufumbuzi wa 6: Kutumia mifano ya kuigwa kuvutia wanawake katika nyanja za kisayansi

Katika nchi za Afrika zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara, wanawake ni wachache sana katika nyanja za kisayansi, jambo ambalo linapunguza upatikanaji wao kwa nyanja zenye faida. Katika nchi nyingine, kuwatambulisha wanawake na wasichana walio balehe kwa mifano ya kuigwa ya kike na hadithi za mafanikio kumeonyeshwa matokeo ya kutia moyo katika kuhimiza wanawake kuingia katika nyanja za kisayansi. Kwa mfano, mgawo wa nafasi za wanawake katika halmashauri za vijiji uliongeza uwezekano wa uongozi wa wanawake na kupunguza pengola matarajio ya kazi za ujuzi wa juu kati ya wasichana na wavulana kwa karibu theluthi moja. Nchini Ufaransa, mpango wa Wasichana katika Sayansi na L'Oréal ultio hutuba darasani kwa saa moja na wanawake vijana wenye taaluma ya sayansi. Tathmini ya kina ya mpango huu ilionyesha kuwa wakati wana sayansi wanawake wanaingilia kati katika madarasa ya shule ya upili, huwa inapunguza dhana potofu zinazohusiana na taaluma za kisayansi kati ya wasichana na wavulana, na huongeza idadi ya wasichana katika mwaka wa mwisho wa shule ya upili kuendelea na programu ya maandalizi ya sayansi.

Ufumbuzi wa 7: Kutoa ujuzi wa kijamii na kihisia

Mafunzo ya Mpango wa Kibinafsi (PI), ambayo yanalenga stadi fulani za kijamii na kihisia kama vile juhudhi za kibinafsi, uvumiliu na utatuzi wa matatizo, yamefaulu katika kuboresha matokeo ya kiuchumi ya wanawake. Nchini Togo, programu ya mafunzo iliandalia wajasiriamali bila mpangilio mafunzo ya kawaida ya biashara au mafunzo ya PI. Ingawa mafunzo ya kawaida yalikuwa na athari ndogo, mafunzo ya PI yaliongeza faida ya kampuni kwa 30% kwa ujumla, na kwa 40% kwa wanawake.

Programu mbili nchini Uganda na Liberia ziliwqapatia wanawake vijana walio na umri wa chini ya miaka 20 mafunzo ya ujuzi wa kijamii na kihisia, kama vile kujengwa kujistahidi na ujuzi wa kupanga, pamoja na mafunzo ya ufundi nchini. Programu zote mbili zilongeza uwezekano wa ajira (+48% baada ya miaka 4 nchini Uganda, +30% baada ya miezi 6 nchini Liberia). Nchini Uganda, programu hizo pia ziloboresha hali ya kujiamini kwa wanawake, na kupunguza viwango vyao vya wasiwasi na umri katika ndoa na mimba za mapema.

Picha 1 – Vikwazo vya kitamaduni kwa ushiriki wa soko la ajira lenye tija la wanawake na baadhi ya ufumbuzi unaoleta matumaini.

Inajumuisha mafunzo ya ujuzi wa kijamii na kihisia

Kutoa mafunzo ya Mipango ya kibinafsi (utendaji, uvumiliu, na kutazama mbele):

+40%
faida kwa wajasiriamali wanawake

+48%
ya uwezekano wa ajira kwa wanawake walio chini ya miaka 20




Sahihisha dhana potofu

Taarifa kuhusu mapato wastani:

+28%
ya wanawake huchagua kazi za kiume kwa kawaida.

Kutoa habari kwa waume kuhusu hali halisi ya kijamii:

+160%
ya wanawake wanatafuta kazi



Tumia mifano ya kuigwa ya kike

Kuwaalika wanasayansi wanawake kuzungumza katika madarasa ya shule ya upili:

+32%
ya wanafunzi wa kike wa shule ya upili huchagua mwelekeo wa kisayansi

Kuajiri wakufunzi wa kike

Kuajiri wakufunzi wa kike katika Usimamizi Endelevu wa Ardhi:

+60%
katika maarifa **+50%**
katika kuitishwa kwa teknolojia

Sanduku la 1: Kuza ufikiaji wa wanawake katika sekta zinazoibuka, kama vile sekta ya kidijitali na nishati mbadala, ambapo mapendeleo ya kijinsia bado hayajazingatiwa

Hii inaweza kufanywa kwa kurekebisha mafunzo ya wanawake ili kupatana na mahitaji ya sekta hizi au kuongeza ufahamu mionganini mwa waajiri. Ingawa hakuna mradi unaotolewa kwa wanawake tu katika sekta ya kidijitali katika nchi inayoendelea ambaao umetathminiwa kwa kina, tathmini ya athari za programu ya mafunzo ya ufundi stadi ambayo pia ni wazi kwa wanaume, iliyolandaliwa na Gender Innovation Lab ya Benki ya Dunia nchini Nigeria, inatia moyo: ikilinganishwa na kikundi cha kudhibiti, 28% zaidi ya vijana waliohitimu walihamia kwenye sekta ya kidijitali walipopewa mafunzo ya wiki kumi ili kukidhi viwango vya kimataifa. Mabadiliko kuelekea sekta ya kidijitali yanaonekana mara tatu zaidi kwa wanawake walio na upendeleo dhahiri dhidi ya utaalamu wa wanawake (yaani, upatikanaji wa ajira kwa ujumla).

Uzoefu wa hapo awali umetusaidia kutambua baadhi ya ufumbuzi unaopunguza vizuizi vya kawaida vya kijamii katika soko la ajira. Hata hivyo, tathmini zaidi za athari bado zinahitajika si tu kwa ajili ya kuthibitisha ufanisi wa afua hizi katika miktadha tofauti lakin pia kwa ajili ya kufuatilia uwezekano wa matokeo yasiyotarajiwa, kama vile ongezeko la unyanyasajji nyumbani.

Kwa maelezo zaidi na marejeleo yaliyotumika kwa muhtasari huu, tafadhali rejelea ripoti kamili ya kiufundi hapa: [Resource Home | AFD – Agence Française de Développement](#)

Bibliografia

ILO (2018), *Women and men in the informal economy: A statistical picture*, 3rd ed., Geneva.

World Bank Group (2019), *Profiting from Parity: Unlocking the Potential of Women's Business in Africa*, World Bank Group, Washington, D.C..

World Bank (2022), *Breaking Barriers: Female Entrepreneurs Who Cross Over to Male-Dominated Sectors*, World Bank, Washington D.C.

Mbirianjau L. W., Chege F. and Oanda I. (2019), « Exploring Enabling Interventions for Increasing Female Students' Access and Participation in Science, Technology, Engineering and Mathematics (STEM) Disciplines in Kenyan Public Universities », *Msingi Journal*, 1(2), 1-6.

Jayachandran S. (2021), « Social norms as a barrier to women's employment in developing countries », *IMF Economic Review*, 69(3), 576-595.

Goedhuys M., Mahé C., Nillesen E. and Reitmann A. (2023), « Measuring social norms towards women and work in Tunisia: An assessment of the 'opinion-matching' method », *Working Paper, AFD, Paris*.

